

## **Kwanini Watu Huanguka Kutoka Kwenye Neema**

Kwa Lugha dhahiri na ya kimfano, mtume Petro anatutahadharisha wakristo kwamba tusiruhusu machafu ya ulimwengu huu yatunase, 2 Petro 2:20-22 na kutuvuta kutoka kwenye neema. Lakini bado, hata pamoja na maonyo yote ya kwenye maandiko kuhusiana na kuanguka, twaanguka. Ni kwanini?.

Katika mfano wa mpanzi Yesu anaeleza kuwa watu wataanguka kutoka kwenye neema kwa sababu ya shughuli za dunia, udanganyifu wa mali, maingiliano na ulimwengu huu na anasa za dunia, Mathayo 13:18-23. Hivi karibuni, shirika kubwa la uchapaji liliwafanyia utafiti watu wapatao 5,000 waliodaiwa kuanguka kutoka kwenye neema, na yafuatayo ni baadhi ya matokeo ya utafiti huo.

59% ya watu walionguka kutoka kanisani walilaumu mabadiliko ya maisha. Mabadiliko kama vile ya kuhamia mji mwingine, kuanza kazi mpya, kutilikiwa, Ni kweli kwamba baadhi ya mabadiliko katika maisha ni magumu sana na hupelekea msongo wa mawazo. Wanadai kwamba talaka, ukata na kuhamia mji mwingine ni baadhi ya mambo yanayopelelea familia kuwa na msongo wa mawazo. Lakini kama tumeijenga nyumba yetu katika Kristo, Mathayo 7:24. Na wakawa wanaendeleza imani inayotutaka tuwe “Hodari, msitikisike, mkazidi sana kuitenda kazi ya Bwana...” 1 Wakorintho 15:58. Basi haitajalisha ni mabadiliko gani yanatujia; Kristo bado ni kipaumbele chetu cha kwanza. Labda ndiyo maana 59% ya watu huanguka kutoka kwenye neema. Siyo kwa sababu ya mabadiliko ya maisha bali ni matokeo ya imani isiyo na mizizi.

19% ya watu wanaoanguka kutoka kanisani walidai kwamba walikuwa wametingwa tu hata wakakosa muda kwa ajili ya Mungu. Kwa sababu yapo mengi yanayoendelea na wakaruhusu uaminifu wao kwa Mungu kuwa mhanga wa kwanza. Tumefundishwa waziwazi kwamba tunapaswa kuukomboa wakati, Waefeso 5:16. Namna mojawapo ya kuukomboa wakati ni kuwa wakili mwaminifu kwa kila dakika ambazo Mungu anakupa. Mtu ye yote na kila mtu anaweza kudai kuwa alitingwa na kitu chochote. Kwa mara nyingine, hili huonyesha tatizo kwenye kuweka vipaumbele. Hivi ni kweli tumetingwa sana hata kukosa muda wa kumheshimu Mungu? Tumetingwa sana hata hatuna muda wa kumwabudu Mungu? Tumetingwa sana hata kutokuwa na muda wa kumwabudu aliyetufia? Kama ndivyo, basi tumetingwa sana hata hatuna muda wa kwenda mbinguni

17% ya watu walioanguka kutoka kanisani walidai kuwa walianguka kwasababu ya majukumu ya kifamilia/nyumbani. Waliwaacha watoto wakabanwa na masuala

ya shulen. Ama walitumia muda mwangi kufukuzia ligi za soka, wakitumaini kupata ufadhilli siku moja. Na wengine walidai kuwa walitingwa na kuwahudumia wazazi wao ambao wamezeeka. Inanisononesha kuona kwamba watoto wetu wengi wanapotelea ulimwenguni. Inaniogofya kufikiria kwamba hata wa kwangu watazoza. Uhalsia ni kwamba wazazi tulio wengi tumetingwa na shughuli za dunia kuliko kuwalea watoto wetu kwa ajili ya kukabiliana na ulimwengu unaokuja. Ndiyo, tunatakiwa kutoa chakula, mavazi, mapambo na huduma za kiafya na mengine yaliyo ya lazima, 1 Timotheo 5:8. Lakini tuisahahu lililo bora zaidi-kuwalea katika “adabu na maonyo ya Bwana,” Waefeso 6:4

7% ya watu waliofanyiwa utafiti walidai kuwa waliacha kanisa kwa sababu hawakuwa wanajisikia vizuri na kanisa. Wengine walitaja mambo fulani kuhusu muhubiri na wengine walizungumzia tabia mbovu za waumini, na wengine walisema kuwa kusanyiko walilokuwa wakihuduria lilikuwa na ubinafsi mwangi. Ni dhahiri kwamba inawezekana kuna watu mionganoni mwetu ambao wametenda dhambi na wanotenda dhambi mionganoni mwetu. Unaweza kuamini hilo? Ni dhahiri pia kwamba kuna makusanyiko ambayo watu kwa makusudi wengine bila kukusudia wanakuwa wabinafsi. Na watu wanapoanguka kutoka katika mikono ya Mungu, kutoka kwenye neema kwa sababu ya mambo haya, hivi si wanampita swala dume? Au wanafanya “mchezo wa lawama” ili kuhalalisha kuanguka kwao kutoka kwenye neema?

Ndugu, unaweza kuchunguza maandiko juu na chini, na hutakuta sababu ya kuhalalisha anguko la kutoka katika neema. Hakuna sababu ya kuanguka kutoka kwenye neema, ni udhuru wenyewe kilema tu.